

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI

HALMASHAURI YA WILAYA YA NJOMBE

TAARIFA YA KUKABIDHI MRADI WA UJENZI WA SKIMU YA UMWAGILIAJI ITIPINGI

29TH SEPTEMBER, 2017

MKATABA NAMBA. LGA/031/2016 - 2017/W/02 LOT No.01

KANDA YA UMWAGILIAJI MBEYA

S.L.P 3575

MBEYA

HALMASHAURI YA NJOMBE

S.L.P 547

NJOMBE

- **UTANGULIZI**

Halmashauri ya Wilaya ya Njombe ilipata fedha Tshs 400,000,000.00 mwaka 2016 (Milioni Mia Nne) kupitia mpango wa Small Scale Irrigation Development Project (SSIDP) kwaajili ya ujenzi wa Skimu ya Umwagiliaji Itipingi. Skimu hii ilifanikiwa kutengewa fedha baada ya Halmashauri kuwasilisha maombi kupitia mfuko wa kuendeleza miradi ya Umwagiliaji Wilayani (DIDF) mwaka 2011/2012.

Mara baada ya kupata fedha Halmashauri ilianza hatua za kimanunuzi kumpata mkandalasi mwenye sifa za kuweza kutekeleza ujenzi wa mradi huu. Baada ya hatua zote kukamilika Mkandalasi M/S Engineering Plus (T) Ltd alikidhi vigezo vya ujenzi wa mradi huu na kusaini mkataba wenye namba LGA/157/031/2016-2017/W/02/LOT No.1 na Halmashauri ya Wilaya ya Njombe. Mara baada ya kusaini mkataba wenye thamani ya Tshs. 388,824,000.00/= Mkandalasi M/S Engineering Plus (T) Ltd tarehe 18th Januari, 2017 alikabidhiwa kazi tayari kwa kuanza ujenzi. Mradi huu unajengwa kwa muda wa miezi nane na kukabidhiwa tarehe 18th septemba, 2017 na mara baada ya kukabidhi mradi utakuwa na muda wa matazamio kwa miezi 12 na baada ya hapo utakabidhiwa rasmi.

- **KAZI ZILIZOPO KWENYE MKATABA**

- Ujenzi wa banio (Headwork)
- Ujenzi wa mfereji mita 1725
- Ujenzi wa vivusha maji viwili (2)
- Ujenzi wa vigawa maji nane (8)

- **UTEKELEZAJI**

- Ujenzi wa banio (Headwork) – umekamilika kwa mujibu wa mkataba
- 2) Ujenzi wa mfereji mita 1725 - umekamilika kwa mujibu wa mkataba
- 3) Ujenzi wa vivusha maji viwili (2) - umekamilika kwa mujibu wa mkataba

4) Ujenzi wa vigawa maji nane (8) - umekamilika kwa mujibu wa mkataba

- **KAZI ZILIZOONGEZEKA**

Zifuatazo ni kazi zilizoongezeka

- Ujenzi wa vivusha maji viwili (2)
- Ujenzi wa kalvati
- Ujenzi wa kivusha maji ya mvua.

5.0 MUDA ULIOTUMIKA

Muda uliokwishatumika Mpaka tarehe 18/09/2017 ni miezi 8 kwa mujibu wa mkataba.

6.0 FEDHA NA MALIPO

Gharama ya ujenzi wa mradi kimkataba ni Tshs. 388,824,000/= ambapo mpaka sasa mkandarasi ameshalipwa kiasi cha Tsh. 306,876,840. Na malipo ya mwisho yatafanywa mara baada ya ukaguzi wa kazi hii kufanyika.

Hata hivyo kipindi chote cha muda wa matazamio (miezi 12) mradi utakuwa chini ya uangalizi wa mkandalasi huku mradi ukiendelea kutumika na walengwa. Ambapo asilimia 5 ya fedha itahifadhiwa kwa mujibu wa mkataba.

- **MCHANGO WA WAKULIMA**

Ifuatayo ni michango ya wakulima katika mradi wa Umwagiliaji Itipingi:-

- Utengenezaji wa barabara kuelekea eneo la mradi na mashambani
- Pia wakulima watachimba mifereji inayoingiza maji kwenye mashamba yao
- Wakulima wameshiriki katika usimamizi wa ujenzi kwa kushirikana na wataalamu kutoka Kanda na wilayani
- Vilevile wakulima walishiriki katika shughuli za upembuzi yakinifu ambapo wameruhusu mfereji kupita kwenye maeneo yao

- **ENEO LA SKIMU**

Eneo la skimu linalofaa kwa kilimo cha umwagiliaji ni hekta 160 ambapo eneo linalolimwa kwa sasa ni hekta 40 eneo linalotegemewa kulimwa mara baada ya kukamilika kwa mradi awamu hii ya kwanza ni hekta 80.


- **CHANGAMOTO**

Kuwepo na mvua baadhi ya siku kulisababisha kazi kutofanyika.

- **USHAURI WA MHANDISI MKAZI.**

- Wakulima wanatakiwa kuutunza mradi kwa kuhakikisha miundombinu iliyojengwa haiharibiwi na kuzuia mifugo isiharibu miundombinu.

Nawasilisha



Eng Saidi Mbiru

Mhandisi Mkazi